TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Kumb na: Taro /P/2022/ A11 **: Swahili Version:** Tarehe: 29 Aprili 2022

**KENYA V TANZANIA KATIKA KULINDA MASLAHI YA WANAMUZIKI (MIITO YA SIMU KWA UMPIGIAE) RING BACK SERVICES**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

***RINGBACK*** *ni muito wa simu anaousikia mpigaji simu kipindi anampigia simu mtu mwingine akisubiria mtu yule apokee.*

## KENYA

Mnamo tarehe 4 Mwezi Aprili 2022, Jamhuri ya Kenya kupitia Raisi wa nchi hiyo, Mh. Uhuru Kenyatta alisaini na kupitisha kuwa sheria mswada wa marekebisho ya sheria ya Hakimiliki **''THE COPYRIGHT ACT (AMENDMENT) BILL, 2021''**. Hatua hii inatafsiriwa kuwa ni mapinduzi katika kuhakikisha maslahi ya wasanii yanalindwa nchini Kenya. Marekebisho hayo ya sheria yamekuja kuongezea kifungu **30C** katika sheria ya hakimiliki Kenya ifahamikayo kama **THE COPYRIGHT ACT.CAP 130. RE. 2014**. Kifungu hicho kipya kimeweka utaratibu wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na mauzo ya kazi za muziki kupitia **miito ya simu kwa** umpigiae **(Ring backs)** kwenye mitandao ya simu. Utaratibu huo unaelekeza kuwa mapato yanayopatikana katika mauzo hayo tajwa hapo juu lazima yagawanywe kwa utaratibu ufuatao:-

1. Mtoa huduma (kampuni inayopeleka kazi za muziki katika mitandao ya simu) itachukua **asilimia saba tu (7%)** ya mapato yote
2. Kampuni ya simu/mawasiliano inayotumia kazi hizo za muziki kama miito ya simu kwa umpigiae itachukua **asilimia kumi na sita (16%)** ya mapato yote

3. Msanii wa muziki au mmiliki wa hakimiliki wa kazi ya muziki atapata **asilimia hamsini na mbili (52%)** ya mapato yote

Kabla ya kuwepo kwa sheria hiyo utaratibu uliokuwa unatumika, ulikuwa kandamizi sana kwa wasanii wa muziki nchini Kenya. Ambapo msanii alikuwa hapati zaidi ya asilimia kumi na sita (16%) ya mapato yote.

Kenya imetumia sheria iliyotungwa na bunge kulinda maslahi ya wasanii wa muziki. Mabadiliko hayo ya sheria yalipitia mchakato wa kuwahusisha wadau mbalimbali kutoa maoni yao ikijumuisha, asasi za kiraia, taasisi za kimataifa zinazoshughulikia maswala ya hakimiliki, watu binafsi, wataalamu wa masuala ya hakimiliki, wasanii na umma kwa ujumla.

**<u>TANZANIA</u>**

Sheria ya Tanzania inatambua mapato ya kwenye mitandao ya simu kupitia miito ya simu kwa umpigiae **(RING BACKS)** kama Mirabaha (Royalties). Mapato hayo yanajulikana kama Mirabaha (Royalties) na sio mauzo (Sales) . **HIVYO BASI** yameingizwa kwenye mfumo wa ukusanyaji Mirabaha na kusababisha wasanii wa muziki kushindwa kuingiza kiasi kikubwa cha mapato kama mauzo. Ingawa msimamo wa sheria uko hivyo lakini kuna utaratibu wa kimazoea ambapo baadhi ya wasanii wakubwa huuza kazi zao za sanaa kwenye mitandao ya simu kama wafanyavyo Kenya. Kwenye utaratibu huo makampuni ya simu huwa yanachukua nafasi ya mtoa huduma na kupata kiasi kisichopungua asilimia 60 ya mapato yote ya mauzo kwenye kazi za muziki za msanii. Utaratibu huo wa kimazoea hauna uhalali mbele ya sheria kwani sheria inaelekeza kuwa mapato kupitia miito ya simu kwa umpigiae **(RING BACKS)** yakusanywe kama mirabaha na makampuni ya simu/mawasiliano. Pia Makampuni ya simu/mawasiliano yanapaswa kuomba leseni ya kufanya kazi ya kukusanya Mirabaha hiyo.

Pia sheria inaelekeza kwamba mtandao wa simu/mawasiliano unapaswa kulipa Ada ya asilimia ishirini na nne (24%) ya mapato yote ya mirabaha inayokusanywa kwenye miito ya simu kwa umpigiae. Mirabaha iliyobaki baada ya kukatwa asilimia 24%, inakatwa tena asilimia thelathini 30% kwa ajili ya kuchangia uendeshaji shughuli za COSOTA kisha iliyobaki ndio inagawanywa kwa wasanii.

*<u>HUU NI MFANO WA MAKATO, KAMA MIRABAHA ITAPATIKANA TSH.1000</u>*

Tsh. 1000 x 24% = **Tsh .240** inapelekwa COSOTA kama Ada na Makampuni ya simu

Tsh. 1000 – Tsh. 240 = **Tsh. 760** inapelekwa COSOTA kama mirabaha na makampuni ya simu

<u>IKIFIKA COSOTA</u>

Tsh. 760 x 30% = **Tsh. 228** kwa ajili ya matumizi ya COSOTA

Tsh. 760 -Tsh. 228 = **Tsh 532** inaenda kugawanywa kwa wasanii kama mirabaha.

Kama Tsh .1000 itapatikana kwenye miraba ya miito ya simu kwa umpigiae, ni Tsh. 532 tu ndio inayoenda kugawanywa kwa wasanii.

***Sheria za kurejea:***

1. Kanuni ya 5(1) ya kanuni ziitwazo Copyright and Neighboring Rights (Copyrighted Works-Communication to the Public) Regulations.Gn. No 29 of 2016
2. Kipenge cha 1(A)(2) cha jedwali la pili la kanuni ziitwazo Copyright and Neighboring Rights (Copyrighted Works-Communication to the Public) Regulations.Gn. No 29 of 2016
3. Kipengele cha 2 cha jedwali la tatu la kanuni ziitwazo Copyright and Neighboring Rights (Copyrighted Works-Communication to the Public) Regulations.Gn. No 29 of 2016
4. Kipengele cha 4 cha jedwali la tatu la kanuni ziitwazo Copyright and Neighboring Rights (Copyrighted Works-Communication to the Public) Regulations.Gn. No 29 of 2016

HITIMISHO

Tanzania tunapaswa kujifunza kutoka Kenya na kuboresha sheria zetu kwa kutumia sheria zilizotungwa na Bunge kulinda maslahi ya wasanii na sio kwa kutumia kanuni, ambazo zinaweza kubadilishwa kirahisi na watu wachache ikitokea wanaamua kuwa sio waaminifu kwa maslahi ya umma.

Tanzania inapaswa kurekebisha kanuni zake na kuondoa mapato ya miito ya simu kwa umpigiae (RING BACKS) katika kundi la mirabaha na kuruhusu kazi za muziki kuuzwa kama miito ya simu kwa umpigiae (RING BACKS), ili wasanii wote wa muziki waweze kupata mapato mapya kupitia mauzo ya kazi za muziki kwenye mitandao ya simu.

Kama Tanzania itarekebisha sheria zake na na kuondoa mapato ya miito ya simu kwa umpigiae (RING BACKS) katika kundi la mirabaha na kuruhusu kazi za muziki kuuzwa kama miito ya simu kwa umpigiae (RING BACKS), Basi iweke utaratibu unaowiana au kufanana na Kenya, wa kuonyesha mgawanyo wa mapato kati ya Msanii au Mmiliki wa Hakimiliki ya kazi ya Muziki, Mtoa huduma na Kampuni za simu.

Tanzania inapaswa kila ikifanya marekebisho ya sheria ya Hakimiliki/ Hakishiriki ishirikishe wadau kwa uwazi ili kuruhusu maoni kutoka pande mbalimbali kwa maslahi ya sekta ya Sanaa.

ASANTENI

MUNGU AIBARIKI TANZANIA, MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA

(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**

**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**